# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 23 Ahadi za Mungu

**SOMA Mwanzo 3:15, 12:1 – 3; Warumi 6:23, 13:15 – 16, 22:17 – 18; Wagalatia 3:16 na 26 – 29; 1 Samweli 7:13 – 14; Luka 1:32 – 35.**

**SOMO**

Mungu ni wa upendo na wa msamaha. Adamu na Hawa walipofanya dhambi, Mungu aliwaadhibu. Lakini aliwapa ahadi ya tumaini kwa siku zijazo. Hii ilikuwa ahadi ya kwanza kwa baadhi ya ahadi zenye Mungu aliahidi wale watu wanaomwamini. Mungu aliahidi kwamba atapeana njia ya kuepuka dhambi na kifo.

Wakati Mungu alikuwa anaambia nyoka, aliambia Adamu na Hawa pia, "Nitaweka uadui kati yako na mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wa wake; ataponda kichwa chako na utamponda kisigino." Mwanzo 3:15.

Haya maneno ni magumu kuelewa, kwa hivyo tunayaangalia kwa umakini. Tutayaangalia kifungu baada ya kifungu.

*Mimi (Mungu) nitaweka uadui kati yako (nyoka) na mwanamke (Hawa).*
Nyoka alikuwa adui wa Hawa kwa sababu alimdanganya akafanya dhambi na akahukumiwa na Mungu kufa. Nyoka anasimamia dhambi na watu waovu.

*Nitaweka uadui kati ya uzao wako (nyoka) na uzao wa mwanamke (Hawa).*
Uzao wa nyoka ni wale watu wanaofanya vile nyoka alifanya. Wanapinga amri za Mungu. Uzao wa mwanamke ni Yesu. Alikuwa na mama wa kibinadamu lakini hakukuwa na baba wa kibinadamu. Baba yake ni Mungu. Watu Hawakumtaka na wakakataa mafundisho Yake.

*Yeye (Yesu) ataponda kichwa chake (nyoka) na wewe (nyoka) utauma kisigino chake (Yesu).*
Watu waovu waliua Yesu. Mungu alimhuisha kutoka kwa wafu kwa sababu hakukuwa na dhambi. Kifo cha Yesu hakikuwa cha muda mrefu kama pigo kwa kisigino, ni uchungu lakini ni kwa muda mfupi.

Kupitia kwa kifo chake, Yesu aliharibu uwezo wa dhambi kwa wale wote wanaomwamini. Hii ndiyo maana ya kuponda kichwa. Hii ni mwisho na ni pigo la kudumu. Kila mtu anatenda dhambi na kwa hivyo anasitahili kufa. Hii ahadi ya Mungu inatupa tumaini kwamba siku moja dhambi na kifo vitaharibiwa. Hii ni tumaini la uzima wa milele.

**Maswali na Majibu**

*1.* Adhabu kwa Adamu na Hawa ilikuwa nini kwa sababu walifanya dhambi?
*Watakufa.*

*2.* Nani ndiye alikuwa uzao wa mwanamke (Hawa) atakayeharibu nguvu za dhambi na kifo? *Yesu Kristo.*

*3.* Jina Ibrahimu lina maana gani? *Baba wa walio na imani.*

*4.* Nani ndiye mzao wa kipekee wa Ibrahimu? *Yesu Kristo.*

*5.* Tunaweza kushiriki kwa ahadi za Mungu kwa Ibrahimu namna gani?
*Kwa kubatizwa na kuwa na imani kwa Mungu.*

*6.* Nani ndiye mwana wa Daudi wa kipekee mwenye Mungu alimwahidi?
*Yesu Kristo.*

7. Kiti cha enzi cha Daudi chenye Yesu atakuja kutawalia kiko wapi?
*Yerusalemu*.

*8.* Mariamu aliambiwa nini yenye inatimiza ahadi za Mungu kwa Daudi?
*Yesu atakuwa Mwana wa Mungu. Atatawala milele kutoka Yerusalemu kwa kiti cha Daudi.*

*9.* Nini itafanyika kwa Daudi wakati Yesu atarudi?
*Atafufuliwa kutoka kwa wafu na ashiriki kwa furaha ya Ufalme.*

*10.* Mungu anatuahidi nini tukiwa na imani?
*Mungu atatuondolea shida zote za dhambi na tuishi milele kwa Ufalme wa Mungu.*

**Mistari ya kukariri**

Mwanzo 3:15 Warumi 6:23 Wagalatia 3:26 – 29 Luka 1:32 – 33

**Mazungumzo**

Zungumza juu ya ahadi zenye Mungu aliambia Ibrahimu na Daudi. Zinatimizwa namna gani? Tunaweza kufanya nini ili tushiriki kwa hizi ahadi?

**Kuandika**

Andika ahadi zenye Mungu aliambia Adamu na Hawa kupitia kwa nyoka. Eleza vile kila kifungu kinatimizwa.

Miaka mingi baadaye, Mungu alizungumza na mtu aliyeitwa Abramu. Alimwambia atoke kwa nchi yake ya Uru na asafiri kwenda nchi ingine yenye Mungu angemwonyesha. Mungu aliambia Abramu ahadi zingine nyingi kwa sababu Abramu alimtii. Mwanzo 12:1 – 3. Mungu aliahidi kwamba wazao wa Abramu watakuwa taifa kubwa. Mungu alichagua Abramu awe baba wa taifa la Wayahudi. Mungu tena alimwambia, hatakuwa wa Wayahudi pekee, lakini, watu wote wa mataifa yote watashiriki kwa hizo baraka. Mungu alibadilisha jina la Abramu na kuwa Ibrahimu, maana yake ni 'Baba wa watu wengi.' Ibrahimu ni baba wa watu wote wa imani.

Baadaye, wakati Ibrahimu alipokuwa akiishi kwa nchi ya Israeli, alikuwa mkarimu kwa mpwa wake Lutu na akamwacha achague sehemu nzuri ya nchi. Mungu aliahidi kwamba atampa Ibrahimu nchi hiyo yote pamoja na wazao wake, milele. Mwanzo 13:15 -16. Ibrahamu kuishi kwa nchi milele ni lazima aishi, kwa hivyo Mungu alikuwa anaahidi Ibrahimu maisha ya milele.

Mungu aliahidi kwamba wazao wa Ibrahimu watakuwa taifa kubwa. Alisema kwamba wazao wa Ibrahimu utakuwa kama nyota, yaani wasiohesabika. Lakini wakati huo Ibrahimu hakuwa na watoto. Ibrahimu aliongoja kuzaliwa kwa mwanawe Isaka kwa miaka ishirini. Kwa hivyo Ibrahimu alikuwa na imani kwa ahadi za Mungu. Mungu alifurahi kwa sababu Ibrahimu alikuwa na imani kwa ahadi zake. Mwanzo 15:5 – 6.

Mwishowe Ibrahimu alipata mwanawe Isaka. Isaka alipokua mkubwa, Mungu alimjaribu Ibrahimu kuona kama anampenda kwa moyo wake wote. Mungu alimwambia Ibrahimu amtolee mwanawe kama dhabihu. Ibrahimu alimpenda Mungu sana na akakubali kufanya hivyo. Mungu alimkataza Ibrahimu asimuue Isaka. Hapo Mungu alifurahi sana kwa sababu Ibrahimu alimpenda sana. Alimwahidi, "Nitakubariki na kufanya wazao wako wawe wengi kama nyota za angani tena kama mchanga wa bahari …. na kupitia mzao wako, watu wa imani wote wa nchi watabarikiwa." Mwanzo 22: 17 – 18.

Karne nyingi baada ya Ibrahimu, mzao wa maana mmoja kutoka kwa uzao wa Ibrahimu alizaliwa. Huyu ni Yesu Kristo. Wagalatia 3:16 inatwambia hivyo. ""Hapa ahadi zilikuwa kwa Ibrahimu na uzao wake. Haijasema, "Kwa wazao", eti wengi, la hasha ni kwa mmoja. "Kwa uzao wako", ndiye Kristo." Yesu alitimiza ahadi za Mungu na ataletea watu wote baraka.

Wagalatia inaendelea kutwambia kwamba, tukiwa na imani na tubatizwe katika Yesu, tunakuwa wazao wa Ibrahimu na tunakuwa na sehemu kwa ahadi za Mungu za uzima wa milele katika Ufalme Wake hapa duniani. Wagalatia 3:26 - 29.

Somo lililopita lilikuwa juu ya ahadi za Mungu kwa Daudi. Daudi alitaka kujengea Mungu Hekalu Yerusalemu. Lakini Mungu akasema mwanawe ndiye atajenga Hekalu. Mungu alifurahia Daudi na akamwambia ahadi kuu. Hizi ahadi zilitimizwa kwa sehemu na mwanawe Sulemani, lakini wakati Bwana Yesu atakaporudi ndiye atatimiza zote.

Mungu aliahidi Daudi mwana wa kipekee. Alisema, "Nitakuwa baba yake na yeye atakuwa mwanangu." 2 Samweli 7:14. Agano Jipya inatwambia vile hizi ahadi zilitimizwa. Malaika alimkujia mzao mmoja wa Daudi, Mariamu, na akamwambia kwamba atapata mwana aliye wa kipekee naye atakuwa Mwana wa Mungu. Malaika alisema, "Roho Mtakatifu atakuja juu yako, nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa hivyo utakayemzaa ataitwa mtakatifu – Mwana wa Mungu." Luka 1:35

Tena Mungu aliahidi Daudi, "Atajenga nyumba kwa jina langu, na kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara. 2 Samweli 7:13. Tena malaika aliambia Mariamu vile huyu Mwanawe atatimiza hizo ahadi zenye Mungu aliambia Daudi. Malaika alisema, "Atakuwa mkuu na ataitwa Mwana wa Aliye juu na Mungu atampa kiti cha enzi cha baba yake Daudi, na atatawala nyumba ya Yakobo milele na ufalme wake hautakuwa na mwisho." Luka 1:32 – 33.

Daudi alijua kwamba mwishowe Mwanawe (Yesu Kristo) atakapotawala kutoka Yerusalemu, atafufuliwa kutoka kwa wafu na ashiriki kwa furaha ya huo ufalme.

Ahadi za Mungu kwa Agano la Kale zinatimizwa katika Yesu Kristo. Mstari wa kwanza kwa Agano Jipya unasema, "Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu." Matayo 1:1.
Injili (Habari Njema) inatwambia vile Yesu alikuja kutimiza ahadi za Mungu. Yesu ni mwanadamu pekee yake aliyeishi na hakutenda dhambi. Yesu alipokufa msalabani, alishinda dhambi na kuchukua matokeo ya dhambi.

Tukiwa na imani kama Ibrahimu na Daudi, tutashiriki kwa ahadi za Mungu. Tunaweza kuwa na nafasi kwa Ufalme wa Mungu wakati Yesu atarudi hapa duniani. Kwa ufalme tutaishi milele. Mungu atatuondolea shida zote za dhambi kwa maisha yetu. Hii ndiyo ahadi ya Mungu ikiwa tutakuwa na imani kwa Mungu na tumpende na kumtii.